*Namba ya Upimaji ya Mwanafunzi:........................................................*

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE**

**05 SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**Muda: 1: 30** **Alhamisi, 26 Oktoba, 2023 Asubuhi.**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, na B zenye jumla ya maswali **matano (05).**
2. Jibu Maswali yote.
3. Andika Namba yako ya Upimaji katika kila ukurasa sehemu ya juu upande wa kulia.

| **KWA MATUMIZI YA MPIMAJI TU** | | |
|---|---|---|
| **NAMBA YA SWALI** | **ALAMA** | **SAHIHI YA MPIMAJI** |
| **1** | | |
| **2** | | |
| **3** | | |
| **4** | | |
| **5** | | |
| **JUMLA** | | |
| **SAHIHI YA MHAKIKI** | | |



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

*Namba ya Upimaji ya Mwanafunzi:.........................................................*

## SEHEMU A (ALAMA 26)

**1.** Chagua herufi ya jibu sahihi kutoka katika machaguo manne (A - D) na andika katika kisanduku.

i) Ipi ni orodha ya wanyama hatari kwa binadamu?

A. Nyuki na nyoka
B. Kipepeo na mjusi
C. Mende na panzi
D. Kipepeo na nyuki

ii) Ukitazama kwenye kioo utaona taswira yako. Tukio gani husababisha kutokea kwa taswira hiyo?

A. Kupinda kwa mwanga
B. Kusharabiwa kwa mwanga
C. Kutengenezwa kwa mwanga
D. Kuakisiwa kwa mwanga

iii) Sikudhani alikuwa akichemsha maji kwenye jagi la umeme. Baada ya dakika 30 maji yote yalichemka na kukauka. Ni badiliko gani la maada lilitokea ?

A. Kimiminika kuwa gesi
B. Gesi kuwa yabisi
C. Yabisi kuwa kimiminika
D. Gesi kuwa kimiminika

iv) Ili mmea uweze kukua unahitaji maji, mwanga wa jua, na joto la wastani. Je, kitu gani kingine kinahitajika?

A. Kivuli
B. Upepo
C. Udongo
D. Hewa



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

v) Nishati ya mwanga hutokana na vyanzo vya asili na visivyo vya asili. Bainisha chanzo kimoja cha asili.

A. Mshumaa
B. Umeme
C. Jua
D. Taa

[ ]

**2.** Jibu vipengele (i) - (v) kwa kuoanisha kazi za mfumo wa mmeng'enyo wa chakula wa binadamu katika **Orodha A** na sehemu husika katika **Orodha B**. Andika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano uliyopewa:

| | **Orodha A** | **Jibu** | **Orodha B** |
|---|---|---|---|
| (i) | Kutoa asidi inayosaidia kuuwa vijidudu kwenye chakula na kusaidia mmeng'enyo wa chakula | ( ) | A. Tumbo<br>B. Mdomo<br>C. Umio<br>D. Utumbo mpana<br>E. Puru<br>F. Ini<br>G. Kuta za tumbo. |
| (ii) | Kuhifadhi chakula kwa muda | ( ) | |
| (iii) | Kufyonza maji na madini. | ( ) | |
| (iv) | Kupitisha chakula kilicholainishwa hadi tumboni | ( ) | |
| (v) | Kuhifadhi mabaki ya chakula | ( ) | |



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

**3.** Jibu vipengele (a)-(e) kwa kuchagua ugonjwa sahihi kutoka kwenye kisanduku na kuliandika katika nafasi iliyoachwa wazi.

| |
|---|
| Saratani, Kichocho, UKIMWI, Tetekuwanga, Malaria, Kipindupindu, Pumu |

**Maswali:**

a) Ni ugonjwa gani unaambukizwa kwa njia ya hewa au kugusana na mgonjwa ?

______________________________________

b) Ni ugonjwa gani unaenezwa na nzi ?

______________________________________

c) Ni ugonjwa gani unasababishwa na plasmodiamu?

______________________________________

d) Ni ugonjwa gani unaenezwa kupitia minyoo kutoka kwa konokono?

______________________________________

e) Ni ugonjwa gani husababishwa na ukuaji usiokua wa kawaida wa seli za mwili ?

______________________________________



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU B (ALAMA 24)

4. Soma kifungu cha habari na kujibu maswali yanayohusiana na kifungu hicho na ujibu maswali katika kipengele (a)-(e):

Kikundi cha wanafunzi watatu wa Darasa la Nne wa shule ya msingi Lokome walifanya jaribio la kuchunguza uotaji wa mbegu katika mazingira ya shule. Walifanya jaribio kwa kuotesha mbegu za mahindi katika makopo mawili yaliyopewa herufi “R’’ na “X’’. Katika kila kopo waliweka aina na kiasi sawa cha udongo. Mbegu zilizooteshwa katika kopo “R’’ zilimwagiliwa maji na kuota baada ya siku tano, wakati mbegu zilizowekwa katika kopo “X’’ hazikumwagiliwa maji na hakuna mbegu iliyoota. Wanafunzi walimuuliza mwalimu wao sababu za mbegu hizo kutoota. Mwalimu aliwataka wajikumbushe hatua za ufanyaji wa majaribio ya kisayansi. Hatua hizo ni kubainisha tatizo, kutengeneza dhanio, kufanya majaribio, kukusanya data, kuchambua taarifa, kutafsiri matokeo na kufanya hitimisho.

**Maswali:**

a) Jaribio lililofanywa na wanafunzi wa shule ya msingi Lokome lilikuwa na lengo gani ?

______________________________________________________________

b) Taja vitu viwili vilivyotumika kufanya jaribio?

______________________________________________________________

c) Kwa nini mbegu katika kopo “X’’ hazikuota ?

______________________________________________________________

d) Kitendo cha wanafunzi kutaka kujua sababu za mbegu kutoota ni sawa na hatua ipi ya jaribio la kisayansi ?

______________________________________________________________



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

e) Umejifunza nini katika jaribio lililopo katika kifungu cha habari ulichosoma ?

____________________________________________________________

**5.** Chunguza picha zifuatazo kisha jibu kipengele (a) – (e).

A



B



**Maswali**

a) Bainisha shughuli zinazoonekana katika kila picha A na B.

A. ____________________________________________________

B. ____________________________________________________

b) Taja jina la kifaa kinachotumika katika picha A na B.

A. ____________________________________________________

B. ____________________________________________________

c) Ikiwa kifaa kinachotumika katika picha A hakitakuwepo, je unaweza kutumia sehemu gani ya mwili kufanya kazi hiyo?

__________________________________________________________



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

d) Vifaa gani vingine vinaweza kutumika kufanya kazi ilivyooneshwa katika picha A? Taja vifaa viwili:

i) ____________________________________________________

ii) ___________________________________________________

e) Vifaa vilivyo katika picha A na B vina umuhimu gani wa kisayansi?

_______________________________________________________________



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org